Kufanya kazi na Washirika

Benki inashughuilka katika shirika 236 za nchi na ulimwengu

Mengi ya matatatizo yanayokumba mtaifa hivi leo hayatambui mikapa. Kwa sababu hii, jumuiya ya kimatiafa inafanya bidii za pamoja dhidi ya magonjwa, uharibifu wa mazingira, vikwazo vya biashara na ufahamu.
Uchambuzi katika kiwango cha juu ulimwenguni unathibitisha kipaumbele cha benki kuhusu bidhaa za umma: magonjwa ya kuambukiza, mazingira, biashara, ufahamu, na ustawi wa kimataifa wa kifedha. Ikiwa ni katika nchi, mikoa, ama katika nyanja ya kiamtaifa, Benki ya dunia inafanya kazi na mashirika yakimataifa na wafadhili, sekta ya kibinafsi, utumisi wa umma, na mashirilka ya kitaalamu na ya taaluma.

Ushirikiano wa Ulimwenguni

> ***Onchocerciasis Control Program (OCP)* [*Mradi wa Kuzuia kuenea kwa Onchocerciasis] ni mojawapo ya ushirikiano wenye kufaulu zaidi wa washiriki mbalimbali katika historia fupi ya maendeleo.**

Mradi wa Kuzuia kuenea kwa Onchocerciasis umefaulu kabisa kuzuia na pia kumeangamiza kabisa upofu wa maji ya mtoni katika sehemu ya nchi 11 yenye watu milioni 35. Ushirikiano mkubwa ulibuniwa mwaka wa 1974, na hivi leo OCP ina mawakilishi kutoka nchi kama 30 za Kiafrika, kampuni ya madawa ya Merck na makampuni mengine ya kibinafsi, mashirika 12 yasiyokuwa yakiserikali, wafadhili 27, na mashirika wafadhili ya Benki ya Dunia, World Health Organization (WHO) [Shirikisho la Afya Ulimwenguni], United Nations Development Program (UNDP) [Programu ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo], na Food and Agriculture Organization (FAO) [Shirika la Chakula na Ukulima]. OCP imefanya zaidi ya kuepusha visa vya kiasi cha kama 600,000 vya upofu, bali imefaulu kuweka wazi maelfu ya eka za ardhi ya ukulima. Mfano mwengine wa ushirikiano wa pamoja wa kimataifa ni Consultative Group for International Agricultural Research (CGIAR) [Mshikano wa Pamoja wa Utafiti wa Kimataifa wa Ukulima], ambayo ni mshiko wa taasisi za utafiti ambayo imeunda na kusambaza kuboresha kwa mimea ya chakula katika nchi zinazoendelea katika miaka 30 iliyopita, shughuli yenye faida ya mda mrefu kwa lisho bora na umasikini wa sehemu za mashambani. Taasisi hizi zimetoa zaidi ya aina 500 za mimea ya ngano ambayo inapandwa kwa sasa katika nchi masikini na imesaidia kuongeza pato la wastani la ngano kwa asilimia 75 katika muda wa miongo tatu.
Ushirikiano mwengine wa muhimu unahusisha:

- Global Environment Facility (GEF) [Taasisi ya Ulimwengu ya Mazingira]
- Global Water Partnership (GWP) [Ushirika wa Ulimwengu wa Maji]
- Prototype Carbon Fund [Hazina Asili ya Kaboni]
- Global Alliance for Vaccines and Immunization (GAVI) [Muungano wa Ulimwengu wa Chanjo na Kinga ya Maradhi]
- Joint United Nations Programme on HIV/AIDS (UNAIDS) [Mradi wa Pamoja wa Umoja wa Mataifa wa HIV/UKIMWI]
- Roll back Malaria [Kuangamiza Malaria]

Kukubali na kutekeleza Malengo ya Millenium ya Maendeleo (MDG) katika mwaka wa 2000 kuliimarisha mojawapo ya ushirikiano mkubwa zaidi ulimwenguni wenye nia ya kufikia malengo saba ya muhimu ya kupunguza umasikini, njaa, magonjwa,na kutojuwa kusoma na kuandika. Lengo la nane—“Kuendeleza ushirikiano wa ulimwengu wa maendeleo“—linatilia nuru jinsi ya kuyafikia yale mengine saba.
Katika Mkakamu wa Udhamini wa Maendeleo wa Monterrey, Mexico mwezi Machi, 2002, kulipatikana makubaliano ya pamoja ya ushirikiano kati ya nchi zilizoendelea na zile zinazoendelea: nchi zinazoendelea zichukuwe jukumu la miradi yao ya maendeleo na kutekeleza sera ambazo

zitawawezesha kufaulu kufikia malengo ya MDG, na mashirika ya shughuli mbalimbali na yale ya shughuli za pamoja yatafanya kazi pamoja kuwasaidia na kuwezekane kuwa na hali ya kubuni namna za kupunguza umasikini na kudumisha ukuzaji.

Benki ni mshiriki wa Elimu kwa Wote. Elimu kwa Wote (EFA), ni kati ya juhudi za kiimataifa zinazotokana na MDG na ni kazi iliyochukuliwa na jumuiya ya kimataifa katika World Education Forum [Baraza la Kimataifa la Elimu] la Aprili mwaka wa 2000 nchini Senegal ilikuweza kuelimuisha "kila mwananchi katika kila jumuiya." Mwezi Novemba 2002 wafadhili walikubali kusaidia nchi saba zinazoendelea katika bara Afrika na Amerika ya Kusini—Burkina Faso, Guinea, Guyana, Honduras, Mauritania, Nicaragua, na Niger—kutekeleza sera zao za elimu zikuwe na matokeo. Kazi na hizi nchi inaendelea ilikubuni uwezo unaohitajika na kuondoa tofauti za udhaminii ambayo kwa sasa inadhaniwa kuwa kama milioni $400 kwa mda wa miaka mitatu ijayo (2003-2005). Hizi nchi ndizo za kundi la kwanza la nchi zinaoendelea kufaidika na Education For All Fast Track Initiative [Juhudi ya Fast Track ya Elimu kwa Wote].
Udhamini kwa nchi saba za kwanza kutasaidia kuwaelimisha watoto wakiume na wakike kama milioni 4 ambao kwa sasa hawawezi kwenda shule za msingi. Zaidi ya hayo, wengi wengineo ambao wenge wacha shule sasa watapata nafasi ya kumaliza masomo ya shule. Kudhamini pia kutasaidia kuwafunza walimu wapya, kulipa mishahara ya walimu, kujenga shule mpya, kusaidia mifumo ya elimu kukabiliana na HIV/UKIMWI, na kutafuta namna nyengine za kuhakikisha kuwepo kwa elimu ya msingi liyobora kwa watoto wote. Ushirika wa Elimu kwa Wote ni ushirikiano mkubwa wa serikali za kitaifa, mishikano ya watumishi ya umma, na mashirika kama vile UNESCO na Benki ya Dunia.

Usimamizi wa Misaada

Benki ya Dunia inafanya kazi pamoja na wafadhili wengine washughuli mbalimabli na wale wa shughuli za pamoja na kikundi kidogo cha nchi zinazoendelea ilikuimarisha usimamizi wa misaada na mbinu zake.
Kuna zaidi ya miradi 63,000 ya maendeleo iliyodhaminiwa na wafadhili ulimwenguni, na kila moja kati yao inasimamiwa kwa matakwa mengni tofauti, mielekezo, na mbinu zilizowekwa ili kulinda mradi na kuhakikisha kwamba msaada unawafilkia masikini.

> ***Utafiti wa Umoja wa Mataifa ulivumbua miradi 1,500 Burkina Faso peke yake na karibu 850 Bolivia.***

Hata hivyo, kazi ya kuandaa repoti za aina mbalimbali za mazingira, uhasibu wa miradi, pamoja na makadirio ya upati wa mahitaji kwa kila mfadhili inaweza kuzilemea nchi zinaoendelea ambazo kwa kawaida rasimali zake ni chache mno. Kwa mfano,

- Katika mradi wa misitu Vietnam, iliwachukuwa wafadhili miezi 18 na wafanyikazi 150 wa serikali kununua magari matano kwa sababu ya tofauti kati ya wafadhili juu ya sera za upati wa mahitaji.
- Bolivia, wafadhili watano waliunga mkono mpango wa kuleta mabadiliko katika umasikini wa nyumbani, lakini kila mmoja alihitaji ripoti ya kivyake ya fedha na ya kiufundi. Ofisa wa serikali aliyeshughulikia mradi aligundua kwamba alitumia karibu nusu ya wakati wake akishughulika na mahitaji ya wafadhili badala ya kufanya kazi ya mpango huo.
- Tanzania, maofisa wa afya waligundua kuwa idadi ya miradi pamoja na mahitaji ya kuwaweka wafadhili, naakushughulikia ripoti zao ni mzigo mkubwa sana kwa serikali.

Ufahamu umeonyesha kwamba uwezo katika nchi zinazoendela unaweza kuimarishwa ikiwa wafadhili wanaweka sawa mipango ya shughuli zao. Mipango ya majaribio imeanzishwa Jamaica, Ethiopia na Vietnam.